

## **JESHI LA POLISI LIMEFANIKISHA UPATIKANAJI WA WANAFUNZI SABA WA KIDATO CHA KWANZA BUKOBA**

**Na. Milka Kaswamila- Bukoba DC**

Baada ya msako mkali uliofanywa na Jeshi la Polisi la Wilaya ya Bukoba kwa kushirikiana na wananchi wa kata ya Ibwera, wanafunzi saba ambao walikuwa hawajawasili kuanza masomo ya kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mwemage wamepatikana na tayari wanaendelea na masomo yao shuleni hapo.



Taarifa hii imetolewa na Mkuu wa Shule hiyo wakati Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mheshimiwa Albert Chalamila alipoitembelea shule hiyo jana tarehe 09.02.2023 akiwa ameambatana na Kamati ya Usalama ya Mkoa huo.



Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mheshimiwa Albert Chalamila amelipongeza jeshi la polisi kwa jitihada hizo na amemtaka mkuu wa shule hiyo apeleleze kujua kama kuna changamoto za kiuchumi zilizopelekea watoto hao kuzuiwa kujiunga na elimu ya sekondari ili waweze kusaidiwa na hatimaye wafikie ndoto zao za kielimu.



**MWISHO**